JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA TARIME

***Unapojibu tafadhali taja:***

Kumb. Na. HWT/LI/08/01 17.01.2025

## TANGAZO LA NAFASI ZA KUJITOLEA.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime anawatangazia Watanzania wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Tarime kuomba nafasi za kazi **Kumi na Nne (14) za kujitolea** kwa Kada ya Afya watakaofanya kazi katika Hospitali ya Wilaya, Vituo vya Afya au Zahanati ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Tarime kama zilivyoainishwa hapo chini:-

| Na. | Kada | Idadi ya nafasi |
|---|---|---|
| 1 | Dereva Daraja la II | 2 |
| 2 | Msaidizi wa Hesabu Daraja la II | 1 |
| 3 | Fundi Sanifu Vifaa Tiba Daraja la II | 1 |
| 4 | Mteknolojia Msaidizi Maabara | 7 |
| 5 | Mteknolojia Maabara Daraja la II | 3 |
| | **JUMLA** | **14** |

### A. SIFA ZA JUMLA KWA KADA YA AFYA:

Waombaji wanatakiwa kuwa na:-

(i) Cheti cha taaluma cha Kada aliyosomea na chuo kinachotambuliwa na Serikali

(ii) Awe amesajiliwa na Baraza la kitaaluma kwa Kada za Afya.

(iii) Awe na Leseni ya taaluma husika.

(iv) Awe na cheti cha Kidato cha Nne/Sita kinachotambuliwa na NECTA.

## B. SIFA ZA JUMLA KWA KADA ZISIZO ZA AFYA:

Waombaji wanatakiwa kuwa na:

(i) Cheti cha taaluma cha kozi aliyosomea cha chuo kinachotambuliwa na Serikali.

(ii) Awe anajua Kiswahili na Kiingereza.

## C. MASHARTI KWA UJUMLA.

i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri wa kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka 45 isipokuwa kwa wale tu walioko kazini Serikalini;

ii. Waombaji wote waambatishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza (Detail Curriculum Vitae) yenye anuani inayotumika, namba za simu zinazopatikana na Anuani ya Barua Pepe (E-mail address) pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika;

iii. Maombi yote yaambatane na vyeti vya Elimu na Taaluma vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya Kidato cha Nne au Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika. **Postgraduate/Degree/Advanced Diploma/Diploma/Certificates, - Cheti cha mtihani wa Kidato cha IV na VI, - Computer Certificate, - Vyeti vya Kitaaluma (Professional Certificate from Respective Boards);**

iv. "Testmonial", "Provisional Results", "Statement of results", hati ya matokeo ya Kidato cha Nne na Kidato cha Sita **(FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.**

v. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi.

vi. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.

vii. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe **26 Januari, 2025.**

viii. ***MUHIMU:*** Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya Elimu, aidha anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa:-

**Mkurugenzi Mtendaji (W),**
**Halmashauri ya Wilaya ya Tarime,**
**S.L.P 16,**
**TARIME.**

xiv. ***Maombi yote ya kazi yatumwe kwa njia ya Posta au yawasilishwe Masjala ya Wazi katika ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime.***

xv. **Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili HAYATAFIKIRIWA.**

xvi. Limetolewa na;

*Simon N. Langoi*

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYA**
**<u>TARIME</u>**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
TARIME